SALA YA JIONI

1† *Kusimama. Shairi la siku lisomwe.*

2† *WIMBO uimbwe.*

3† *Muhudumu aseme:*
Ndugu na dada zangu katika Kristo,
tumekusanyika jioni hii,
kusikia Neno la Bwana wetu,
kusifu Jina lake,
kuomba usamehe kwa makosa ya leo,
na kuweka sisi wenyewe na dunia nzima
katika mikono yake kwa usiku unaokuja.

4 *Muhudumu* Bwana awe nanyi.
Wote **Awe pia nawe.**
Muhudumu Kusaidiwa kwangu kunatoka kwa Bwana,
Wote **Aliyefanya mbingu na dunia.**
Muhudumu Mwenyezi Mungu atupatie salama kwa usiku huu, hata mwisho wake.
Wote **Amina.**

5† *Wimbo wa Biblia au wimbo mwingine. Kwa mufano....*
Katika KUJA, na ONYESHO:
Wimbo wa MARIA (Magnificat) p 22, 23 au 24
Katika UFUFUKO:
Wimbo wa UFUFUKO p 26, 27
Katika nyakati nyingine:
Wimbo wa JIONI p28

6* *Wote waketi au kupiga magoti. Muhudumu aseme:*
Sasa tunyamaze kidogo, tukumbuke matendo, maneno na mawazo yetu katika siku ya leo, tukiomba Roho ya Mungu kutuonyesha yale yasiyofaa....
Kunyamaza kidogo.

7 *Muhudumu aseme:*
Mwana mupotevu alisema:
Nitakwenda kwa Baba yangu na nitamwambia, Nimefanya zambi juu ya mbingu na mbele yako, sistahili kuitwa tena mwana wako.
Sisi vile tuombe usamehe kwa Baba yetu.

Wote waseme:
Baba ya milele, mutoa wa nuru na neema,
tumekosea wewe na jirani zetu,
kwa maovu tuliyoyatenda
na kwa mema tusiyoyatenda.
Tumeumiza mapendo yako,
na kuharibu mufano wako ndani yetu.

Tunasikia huzuni na haya,
na tunatubu zambi zetu zote.
Kwa ajili ya Bwana wetu Yesu Kristo,
utusamehe yote yaliyopita;
na utuongoze kutoka katika giza la zambi,
ili tutembee sawa watoto wa nuru. Amina.

— — — — □ — — — —

8a *Kasisi asimame na aseme:*
Mungu Mwenyezi,
mwenye kusamehe wote wanaotubu kwa kweli,
a*wa*rehemu, a*wa*samehe na a*wa*okoe
kwa zambi ze*nu* zote,
a*wa*sibitishe‡ na a*wa*pe nguvu kwa wema wote,
na a*wa*linde katika uzima wa milele,
kwa Yesu Kristo Bwana wetu. **Amina**.

- - - - - - - - - - - - *AU* - - - - - - - - - - - -

8b *Muhudumu au mutu mwingine asiye Kasisi, akipiga magoti atumie ombi hili.*
Ee Mungu, mwenye rehema,
tunakusihi uwape watu wako waaminifu,
usamehe na salama,
wasafishwe zambi zao zote,
wakutumikie na nia ya utulivu;
kwa Yesu Kristo Bwana wetu. **Amina.**

— — — — — — — — — □ — — — — — — — — —

9† *Kusimama. Zaburi ya Siku, au Wimbo, au moja ya Zaburi hizi:* 4, 31:1-7, 91:1-12, 121, *au* 139:1-12.
Kila Zaburi imalizike na:
Utukufu kwa Baba, na kwa Mwana, na kwa Roho Mutakatifu:
Kama ulivyokuwa mwanzo ulivyo sasa,
hata milele na milele. Amina.

10† *Kuketi.*
Kipande kinachotoka AGANO LA KALE kisomwe.
Musomaji aseme kwanza:
Sikieni Neno la Bwana kama lilivyoandikwa...
Na kwa mwisho aseme:
Neno la Bwana ni taa kwa miguu yetu.
Wote: **Na nuru kwa njia yetu.**

11† *Wimbo wa SIMIONI (Nunc Dimittis) ukurasa 25 au 26,*
au wimbo mwingine.

12 *Kuketi.*
Kipande kinachotoka INJILI au kitabu kingine cha AGANO JIPYA kisomwe. Musomaji aseme kwanza:
Sikieni Neno la Bwana kama lilivyoandikwa...
Na kwa mwisho aseme:
Neno la Bwana ni taa kwa miguu yetu.
Wote: **Na nuru kwa njia yetu.**

13† KUHUBIRI

14† *Watu wasimame kuhakikisha* IMANI YA MITUME
Ninamwamini Mungu, Baba Mwenyezi,
Muumba wa mbingu na dunia.

Na Yesu Kristo, Mwana wake wa pekee, Bwana wetu,
aliyetwaa mwili kwa tendo la Roho Mutakatifu,
akazaliwa na Bikira Maria.
Akateswa zamani za Pontio Pilato,
akasulibiwa, akafa, akazikwa,
akashuka kuzimuni mwa wafu,
akafufuka katika wafu siku ya tatu,
akapanda mbinguni,
anakaa kwa mukono wa kuume wa Mungu,
Baba Mwenyezi,
ndipo atakuja tena kuhukumu wazima na wafu.
Ninamwamini Roho Mutakatifu,
Kanisa katolika‡ takatifu,
ushirika wa watakatifu,
kuondolewa kwa zambi,
ufufuko wa mwili,
na uzima wa milele. Amina.

15 *Kupiga magoti. Muhudumu aseme:*
Tuombe sawa Mwokozi wetu alivyotufundisha.

Wote **Baba yetu, uliye mbinguni,**
jina lako litukuzwe,
ufalme wako uje,
mapenzi yako yatimizwe,
duniani kama mbinguni.
Utupe leo chakula chetu cha kila siku;
utusamehe makosa yetu,
kama tunavyowasamehe waliotukosea.
Usitulete katika majaribu,
lakini utuokoe katika uovu.
Kwani kwako ufalme,
uwezo na utukufu,
milele na milele, Amina.

16* *Muhudumu* Ee Bwana, wewe ni jua na ngabu yangu;
Wote **Sitaogopa katika kivuli cha mauti.**
Muhudumu Umenikomboa, Ee Bwana, Mungu wa kweli;
Wote **Katika mukono wako ninaweka roho yangu.**
Muhudumu Unilinde kama mboni ya jicho;
Wote **Unifiche chini ya kivuli cha mabawa yako.**

17† SALA YA SIKU

18† MAOMBI YA KANISA *Muhudumu:*
Tuombee mataifa, na Kanisa, na walio na magumu.

Ee Mungu, muumba na mulinzi wa watu wote, tunaombea wenzetu wa kila inchi katika mahitaji ya kila aina: njia zako zijulikane duniani, na uwezo wako uonekane kati ya mataifa. (Tunakushukuru kwa...)
(Tunaombea zaidi...)
Ee Bwana kwa rehema yako,
Wote **Usikie kuomba kwetu.**

Tunaombea Kanisa lako duniani; utuongoze na kututawala na Roho yako Mutakatifu, ili wakristo wote wajifunze ukweli wako, na kushika imani katika umoja, salama na haki.
(Tunakushukuru kwa...)
(Tunaombea zaidi...)
Ee Bwana kwa rehema yako,
Wote **Usikie kuomba kwetu.**
Tunaleta mbele yako, Baba mwema, wote wanaokosa salama ya kiroho au kimwili: uwafariji, uwasaidie, uwapatie uvumilivu, na uzalishe mambo mema kutoka mateso yao.
(Tunakushukuru kwa...)
(Tunaombea zaidi...)
Baba mwenye rehema
Wote **Ukubali maombi haya**
kwa ajili ya Mwana wako
Mwokozi wetu Yesu Kristo. Amina.

B*adala ya kueleza mengi kwa Mungu, muhudumu anaweza kunyamaza kidogo katika kila sehemu, ili watu waombe kwa kimya.*

19* *Muhudumu anaweza kusema moja au zaidi ya sala hizi:*

Ee Mungu,
hivyo kwako yanatoka matumaini matakatifu yote,
mashauri mema yote, na matendo ya haki yote;
Utupe sisi watumishi wako,
salama tusiyoweza kupewa na dunia;
ili tuzishike amri zako kwa mioyo yetu,
na tukiondolewa woga wa adui zetu,
tukae kwa salama chini ya ulinzi wako,
siku zetu zote;
kwa kustahili kwake Yesu Kristo, Mwokozi wetu.
Amina.

Bwana, uwe mutawala wa nyumba hii;
ufukuze mbali udanganyifu wote wa yule Muovu;
malaika zako wawe walinzi wa salama yetu;
na furaha yako ikae nasi daima;
kwa Yesu Kristo Mwokozi wetu. **Amina.**

Uwe nasi, Ee Baba mwenye rehema,
katika saa za utulivu za usiku huu,
ili sisi, tunaochoka na magumu ya dunia hii isiyodumu,
tupumzike katika uaminifu wako
unaodumu milele,
kwa Yesu Kristo Bwana wetu. **Amina.**

Utuongoze, Ee Bwana, tukikesha,
utulinde, Ee Bwana, tukilala usingizi:
ili tukiwa macho, tukeshe na Kristo;
au tukiwa katika usingizi, tulale salama. **Amina.**

20* *Maombi mengine yanaweza kusemwa.*

21* *Muhudumu* Kuliko walinzi wanaongoja asubui
Wote **Nafsi yangu inangoja Bwana.**

22 SALA KWA KUSAIDIWA KATIKA HATARI
Wote **Bwana, tunakusihi,**
nuru yako iangaze katika giza letu;

na kwa rehema zako kuu,
utulinde katika hatari zote za usiku huu;
kwa mapendo ya Mwana wako wa pekee,
Yesu Kristo. Amina.

23† *Wimbo na kupokea sadaka.*

24 *Baraka au Neema.*

— — — — □ — — — —

BARAKA - *Kasisi:* Tuombe.
Mungu Mwenyezi,
Baba na Mwana na Roho Mutakatifu,
awabariki, awalinde, na akae nanyi,
katika usiku huu, na milele. **Amina.**

- - - - - - - - - - *AU* - - - - - - - - - -

NEEMA - *Watu wote*
Neema ya Bwana wetu Yesu Kristo,
na mapendo ya Mungu Baba,
na ushirika wa Roho Mutakatifu,
ukae nasi sote, milele na milele. Amina.

— — — — — — — — — □ — — — — — — — — —

25* *Wimbo wa kumaliza ibada.*